

## Mapendekezo

1. Tungependa mwongozo wa sera ya kilimo cha mwani na biashara yake kutukinga kutoka kwa wawekezaji na wafanyi biashara fidhuli. Soko liwe huria ili kuzidisha mashindano baina ya wanunuzi.
2. Mwongozo wa kilimo cha mwani unahitaji kuwa na masharti ya kumlinda mwekezaji kutoka kwa uvuvi haramu na haribifu.
3. Matakwa yetu in kwamba kilimo cha mwani kitambuliwe kama shughuli mojawapo ya maduhuli mbadala na ijumuishwe kwenye sera na mipango ya kitaifa ya kuondoa umaskini na kufikia maendeleo ya millennia.
4. Twahitaji mafunzo ya biashara na uwekezaji ili tuongeze ujasirimali na uzalishaji.



Ofisi ya IUCN (muungano wa uhifadhi duniani) ya afrika mashariki na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafiti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS(shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendelevu wa chuma riziki. Uchapishaji wa brosha hizi ni matokeo ya kazi hiyo.

Warsha za jamii ni sehemu mojawapo ya mradi mkubwa "uhifadhi kiini cha mali kwa chuma riziki katika afrika mashariki" unaofadhiliwa na IDRC (kituo cha kimataifa cha utafiti na maendeleo) na Ford Foundation. Pia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha sera za kuwaezesha jamii ya pwani kusimamia rasilimali zao za bahari katika afrika mashariki unaofadhiliwa na KNCF (mfuko wa fedha wa Kiedanren wa kuhifadhi viumbe). Madhumuni ya miradi hii ni kuongeza maarifa na ufahamu juu ya uhifadhi wa bioanuai unavyochangia chuma riziki na kuwasaidia jamii kudhihirisha umuhimu huu kwa wanasiasa na waundaji sera.

Maoni yaliyotolewa kwa chapisho hili si lazima kuwa mawazo ya mitizamo ya IUCN, IDRC, The Ford Foundation, KNCF, CORDIO au EAWLS.

Sifa kwa picha: Sue Wells/IUCN  
TCZCDP

## Kujenga Uwezo wa Jamii Kusimamia Rasilimali ya Baharini Tanzania



## Kundi la Kilimo cha Mwani



Na:  
Rehema Jumaa  
Sheha H Faki  
Hadiya Juma  
Rashid M Haji

## Utangulizi

Kilimo cha mwani kinazidi kuwa muhimu kwa maduhuli na mapato mbadala, hasa kwa wanawake katika vijiji vingi vya pwani ya Tanzania.

Warsha ya kitaifa ya jamii ya pwani ilifanyika Tanga kuanzia tarehe 28 hadi 31 Januari 2008. Lengo la warsha

lilikuwa kuzipa jamii za pwani fursa ya kutangamana na kubadilishana uzoefu wa usimamizi na utendaji kwenye rasilimali za baharini pamoja na kuelezea kwa ufasaha mahitaji yao. Kama wakilishi wa kikundi cha kilimo cha mwani, tulitoa maoni yetu, malengo, shughuli, masuala nyeti na mapendekezo katika mukano huo.

## Vikundi vya kilimo cha mwani, malengo na azma yao

JINA LA KUNDI	MALENGO/SHAUKE
KAMATI ZA USIMAMIZI MTANGA'TA – SAHARE Tanga	<ul style="list-style-type: none"><li>Idihinisha ustawi wa mtandao wa kuhifadhi wa jamii</li><li>Kuimarisha chuma riziki kwa jamii kuititia upunguzaji wa uharibifu wa maliasili za bahari</li><li>Kupunguza na kuondoa umaskini mionganini wa jamii</li></ul>
SHIRIKA LA WAKULIMA WA MWANI KIJIRU LTD Tanga	<ul style="list-style-type: none"><li>Tumainisha kamati kuijandaa kufanya na kuzingatia maduhuli mbadala wa kilimo cha mwani kuititia kilimo cha mwani, ufugaji nyuki, uzalishaji asali na kustawisha mikoko</li><li>Kuboresha hali ya maisha na chuma riziki kwa wanachama</li><li>Endeleza kilimo cha mwani (aina ya kotoni), ufugaji wa nyuki na uzalishaji wa asali, upanzi wa kustawisha mikoko</li></ul>



## Utenzi wa jamii mintarafu ya matumizi endelevu ya rasilimali za bahari

- Shughuli za kuchuma riziki na maduhuli mbadala zimeanzishwa katika maeneo mengi ya pwani ya Tanzania. Hii ni pamoja na kilimo cha mwani, ufugaji wa kaa, chaza, utalii mfumo wa ikolojia na kijamii, ufugaji wa nyuki na uzalishaji asali na shughuli zisizo za bahari kama vile usimamizi wa bustani ya miche, ufugaji kuku, zaraa na biashara ndogo ndogo.

## Maswala kipaumbele

- Biashara ya mwani ina ukiritimba. Uhodhi wa wanunuzu umechangia mashirika machache tu kupewa leseni na kuidhinishwa na serikali ya Tanzania. Leseni hizi zinatumika sehemu maalum peke yake.
- Ukiritimba wa mashirika umeweka na kusababisha bei kuwa chini na sisizo thabiti.
- Serikali ya Tanzania hajatambua kilimo cha mwani kama kitega uchumi mbadala. Kwa hivyo, hajatilia mkazo na kuweikwa katika mipango yake ya maendeleo ya serikali.
- Tuna ukosefu wa pembejeo muhimu za kuimarisha kilimo cha mwani.
- Tuna mgogoro na wavuvi juu ya zana haramu za wavuvi kama vile sumu, juya na mashua zinazoharibu ugwe wa mwani.
- Mabadiliko ya hali ya anga yanayoleta mvua nyingi.

